

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI

OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO – KITENGO CHA UHUSIANO



TAARIFA KWA WANAJUMUIYA YA MUHAS

WAFANYAKAZI BORA WA CHUO KWA MWAKA 2021

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Prof. Andrea Pembe, anapenda kuwatangazia wanajumuiya wote wa MUHAS kuwa wafanyakazi bora wa Chuo kwa mwaka 2021 ni: -

1. **Prof. Karim Premji Manji** – kwa Watumishi Wanataaluma
2. **Bw. Hemed Selemani Mtana** – kwa Watumishi Waendeshaji.

Prof. Karim Premji Manji ni Profesa katika Idara ya Magonjwa ya Watoto katika Shule ya Tiba. Alichaguliwa kutokana na utendaji kazi wake, ubunifu, ubora wa huduma anayotoa na moyo wa kujituma katika kazi mbalimbali hususan katika kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika fani yake. Aidha, kwa kushirikiana na watumishi wengine wa MUHAS, mtumishi huyu amehusika katika kusaidia MUHAS kutambulika kimataifa kupitia tafiti mbalimbali ambazo amekuwa akizisimamia katika Chuo chetu na kuwezesha jamii ya watazania na wanataaluma kunufaika kupitia tafiti hizo.

Bw. Hemed Selemani Mtana ni Mhudumu Daraja la 1 katika Shule ya Afya ya Kinywa na Meno. Alichaguliwa kutokana na utendaji kazi wake, ubunifu, ubora wa huduma anayotoa kwenye ofisi yake hususan katika Kliniki ya Meno. Aidha, amehusika katika kusaidia wateja wa Kliniki ya Meno kupata huduma bora kwa kutimiza wajibu wake wa kuwezesha walimu, madaktari, wanafunzi kuwa na mazingira mazuri ya utoaji huduma bora kwa wagonjwa wanaopata tiba katika Kliniki pamoja na wadau mbalimbali wanaotembelea Shule ya Afya ya Kinywa na Meno.

Wafanyakazi Bora wa Mwaka 2021, watapewa zawadi ya fedha taslim Shilingi Milioni Moja kila mmoja pamoja na cheti cha kutambua mchango wa kazi wanazozifanya. Pia wafanyakazi hawa watapata nafasi ya kushiriki sherehe za Mei Mosi kitaifa Mwanza ambapo Mgeni Rasmi atakuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili unapenda kuwapongeza Prof. Karim Premji Manji na Bw. Hemed Selemani Mtana na kuwatakia kila la kheri katika Utendaji kazi wao.

Imetolewa na:

KITENGO CHA UHUSIANO, MUHAS

29 Aprili 2021